Jamhuri ya Kiarabu ya Misri
Tarehe 12 Mwezi Rajab 1444 Hijry
Wizara ya Waqfu
3 Februari 2023

(١)

# منهج القرآن في عمارة الكون

# Qur’an tukufu na njia yake katika kuimarisha Ulimwengu

**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa Ayman Alasar**

**Kitivo cha lugha na ufasiri**

Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu Bwana wa viumbe vyote, asemae ndani ya kitabu chake kitukufu: { **Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo ili kuiimarisha**} na ninakiri kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa peke yake hana mshirika, na ninakiri

kwamba bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu shusha rehma, amani na baraka kwa Mtume na jamaa zake na maswahaba zake, na mwenye kuwafuata kwa wema mpaa siku ya malipo. Ama baada ya hayo:

Kwa hakika Qur’an tukufu ni kitabu cha Mwenyezi Mungu chenye miujiza ya kudumu, mwenye kusema kupitia Qur’an basi husema kweli, na mwenye kuhukumu kwa Qur’an basi hufanya uadilifu, nacho ni kitabu ambacho wanachuoni hawatoshekinacho, na maajabu yake hayeshi, majini walipoisikia hawakucha kusema: { **Hakika sisi tumeisikia Qur'ani ya ajabu! Inaongoza kwenye uwongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu Mlezi.**}na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: { **Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye ya yaliyo nyooka kabisa, na inawabashiria Waumini ambao wanatenda mema ya**

**kwamba watapata malipo makubwa** }na anasema Mtume (S.A.W) “Hakika Mwenyezi Mungu ana vipenzi katika watu, maswahaba wakauliza: ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni kinani hao? Akasema: Hao ni watu wa Qur’an amewachagua Mwenyezi Mungu na akawapenda kwa mahususi} na anasema Mtume (S.A.W) “ Mbora wenu ni mwenye kufundisha Qur’an na akaifundisha”.

Na Qur’an tukufu imesisitiza sana kuendeleza Ulimwengu, Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuumba mwanadamu na akamdhalilishia ulimwengu na vilivyomo ndani yake ili autengeneze na kuuendeleza, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { **Na akafanya yakutumikieni majahazi yanayo pita baharini kwa amri yake, na akaifanya mito ikutumikieni. Na akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu, na akaufanya usiku na mchana kwa**

**manufaa yenu**.} na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu amevidhalilisha kwenu viliomo katika ardhi, na marikebu zipitazo baharini kwa amri yake, na amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye huruma kwa watu, Mwenye kurehemu.**} na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { **Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri**}.

Na mwenye kuizingatia Qur'an tukufu anaikuta imejaa aya zinazojulisha umuhimu wa kuujenga na kuuendeleza Ulimwengu, na makatazo makali ya kuuharibu kwa njia yoyote, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { **Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo ili kuiimarisha**}kwa maana: amewataka

kuiimarisha na kuindeleza. Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { **Na wenye kuamini na wakatenda mema haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika**} Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **{ basi watakao mchamngu na wakatengenea haitakuwa khofu kwao, wala hawatahuzunika**}Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { **Na katika watu yupo yule ambaye maneno yake kwa maisha ya kidunia hukufurahisha; naye humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ndiye mkubwa wa ukhasimu. Na anapo tawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi.**}.

Na njia ya Qur'an katika kuimarisha Ulimwengu inakusanya aina zote za maendeleo, marekebisho na ujenzi, miongoni mwa aina hizo ni kuzunguka Duniani na kutembea katika pande zake, kutafuta utajiri wake na

kheri mbalimbali alizoziweka Mwenyezi Mungu: anasema katika Qur'an tukufu: {**Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa**} na anasema Ibnu Katheer Allah amrehemu: (Mwenyezi Mungu anazitaja neema zake kwa viumbe wake katika kuwadhalilishia Dunia kwa kuifanya sehemu tulivu haiyumbi wala kutikisika kwa sababu ya milima aliyoiweka, akatoa chemchem, na akatengeneza njia, na akawawekea manufaa na maeneo ya kilimo na matunda, hivyo kunapasa kusafiri na kutembea katika pande za Dunia ili kutafuta riziki).

Amri ya kutembea Duniani ili kuiimarisha imekuja baada ya kutekeleza ibada, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu

kuhusu swala ya Ijumaa: { **Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua. Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa**}.

Na bwana wetu Uraku bin Malik (Allah amuwie radhi) alikuwa akimaliza kuswali Ijumaa husimama mlango wa msikiti na kusema: (Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nimeitika wito wako, na nimeswali faradhi yako, na nimetawanyika kama ulivyoniamrisha, basi niruzuku kwa fadhila zako na wewe ndio mbora wa kutoa riziki).

*     *     *

Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, na rehma na amani zimuendaa Mtume na Nabii wa Mwisho, bwana wetu Muhammad (S.A.W), na ali zake na swahaba zake wote.

Wito wa Qur'an wa kuimarisha Ulimwengu unahitaji jitihada katika kilimo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema : { **Na Ishara hiyo kwao - ardhi iliyo kufa, nasi tukaifufua, na tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila!. Na tukafanya ndani yake mabustani ya mitende na mizabibu, na tukatimbua chemchem ndani yake,Ili wale matunda yake, na hayo hayakufanywa na mikono yao! Basi je, hawashukuru**?}, na anasema , Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Hebu mtu na atazame chakula chake. Hakika Sisi tumemimina maji kwa nguvu, Tena tukaipasua pasua ardhi kwa nguvu, . Kisha tukaotesha humo nafaka, Na zabibu, na mimea ya majani Na mizaituni, na mitende. Na**

**bustani zenye miti iliyo songana baraabara. Na matunda, na malisho ya wanyama; Kwa manufaa yenu na mifugo yen**u}.

Na Mtume S.A.W amebainisha fadhila za kuimarish Ulimwengu kwa kilimo aliposema: (Hakuna Muislamu yoyote anaelima mmea au kupanda mti na akala katika mti huo au mmea huo mwanadamu au myama, isipokuwa huwa ni kama ametoa sadaka), na anasema Mtueme S.A.W: (Kikisimama kiyama, na katika mkono wa mmoja wenu kuna mbegu, akiweza kuzipanda kabla ya kusimama kiyama basi azipande).

Pia Qur'an inatutaka tufanye kazi kwa ufanisi, sawasawa kazi za viwanda, maofisini au kazi za ufundi, na inatutaka kuchunga misingi ya tabia katika biashara, kusaidiana na kuhurumiana.

(١٠)

Ewe Mwenyezi Mungu ilinde Misri yetu na inyanyue bendera yake Ulimwenguni.